Kwa Jina La Allaah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

25/= Ksh

Volume 4, Issue 4

20th Dhul-Hijjah 1431

26th November, 2010

Yaliyomo

Ni UWAHABI Upi Uliokusudiwa? 1– 4

Fadhla Za Mwezi Wa Muharram 4

NI "UWAHABI" UPI ULIOKUSUDIWA?

Mtayarishi: S'ad Shuway'ir

Ni ubora kwangu nimueleze msomaji sababu zilizonifanya niandike makala haya, Marekebisho ya makosa ya ki-Historia kuhusu "Uwahabi", kwani Allaah (*Subhaanahu wata'aalah*) amekifanyia kila kitu sababu zake. Mjadala ufuatao uliozalisha ushawishi wenye majadiliano yenye misingi ya ki-elimu, mazao na mazungumzo yenye muongozo mzuri, ndio sababu za matayarisho yangu ya kuandika makala haya.

Katika mwaka wa 1407H, mimi nilihusika kwenye shughuli muhimu za kibiashara kwenye nchi ya Mauritania, na baadae tukaruka na ndege kuelekea nchini Senegal, na jadwal ya ndege ikatulazimu sisi kubaki katika nchi ya Ufalme wa Morocco kwa muda wa siku sita.

Na katika mojawapo ya masiku hayo, nilikuwa pamoja na mwalimu mmoja wa Chuo Kikuu hapo aitwae Doctor 'Abdullaah. Na katika kikao fulani, tukiwa ndani ya maktaba yake, mijadala chungu nzima ilifanyika. Kutokana na mapenzi yake ya Ufalme unaotawala, na kujumuika kwake katika mikutano ya pale nchini, aliniuliza suala lifuatalo mbele ya wale waliokuwa wamehudhuria ambao idadi yao ilikuwa takriban mashekhe kumi na mbili, wanaotokamana na watu watukufu (yaani - "wamiji").

Akasema, "Sisi twaupenda Ufalme, na roho za Waislamu pamoja na nyoyo zao pia wako tayari kujitolea kwa hali na mali kwa ajili yao, na baina yetu sisi na wewe kuna mafungamano makubwa na mapenzi ya hali ya juu, na utashangaa kuona jinsi watawala na wanavyuoni katika Ufalme huu walivyotanguliza *ikhlaas* kwa juhudi kubwa, malengo yao ni kuukusudia Uislamu na Waislamu. **Lakini, ni ubora ulioje lau kama nyinyi nyote mungelijiepusha na haya madh-hab ya Uwahabi (Wahaabiyyah), ambao umekuja kuwatenganisha na kuwafitini Waislamu?!"**

Kwahivyo mimi nikamjibu kwa kumwambia, "Pengine huwenda ukawa na mawazo yasiyo saheeh, yaliyopatikana kutoka kwenye asili yenye makosa, lakini, tungelipenda kuikaribisha mada hii, mbele ya hadhara ya ndugu zetu, ijadiliwe juu ya misingi ya ki-elimu, yenye kuandamana na ushahidi mpaka fahamu zetu zikubaliane…"

Kisha nikasema, "Na kwa vile kila mwana-adamu huridhika na kuburudika moyo wake, kwa yale yaliyoandikwa na Wanavyuoni wa kwao (wa nchi yao), basi katika majadiliano haya, mimi sitovuka nje ya kumbukumbu zilizo kwenye maktaba hii iliyozungukwa na hizi kuta nne, kwa sababu kama

NI "UWAHABI" UPI ULIOKUSUDIWA?

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

munionavyo, mimi sikubeba hata kitabu kimoja, na wala sikuutarajia mdahalo huu.

Na kwahivyo, kabla hatujaanza, natumai yakwamba mdahalo huu hautofungamana na ukaidi, wala uzalendo, au kutoa rai zisizokuwa na ushahidi usioridhisha wa kutilia nguvu, kwa sababu kutafuta ukweli ndilo lengo letu, na muafaka na Amri ya Allaah na amri ya Mtume wake (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*) ndicho kikomo chetu, na kuinusuru Dini ndilo tumaini la matumaini tulo nayo."

Akasema: "Mimi nakubaliana na wewe katika jambo hilo, na hawa mashekhe waheshimiwa ndiwo watakaokuwa mahakimu baina yetu sisi."

Nikasema, "Hayo yameniridhisha, sasa baada ya kujitegemeza kwa Allaah nakusubiri ulete utangulizi katika mdahalo huu (Debate)."

Akasema, "Hebu chukulia kwa mfano, maneno aloyasema al-Wanshareesi katika kitabu chake kiitwacho al- Mi'yaar juzuu ya 11, ambayo ni: Al-Lakhami aliulizwa kuhusu watu waliokuwa wakiishi katika sehemu ambayo ma-Wahabi walijenga msikiti, ni nini hukmu ya kuswali kwenye msikiti huwo?

Napenda kuwadokezea hapa yakwamba: Kitabu hiki al-Mi'yaar, ni kitabu kilichokusanya fatwa kutoka katika Fiqh za Imaam Maalik, kilitungwa na Ahmad bin Muhammad al-Wanshareesi, na kikachapishwa katika juzuu 13, na kuchapishwa na Serikali ya Morocco, kisha chapa hizo zikagawanyizwa kwa njia ya misaada.

Baada ya kuwasilishwa kwa suali hilo, na kukileta kitabu mbele ya hadhara, juzuu ya 11, nikajibu kwa kusema: Yakwamba fatwa kuhusu suali hili ni sawa, nasi twakubaliana na al-Lakhami kuhusu yaliyotajwa katika fatwa yake.

Akasema, "Kwahivyo tumeafikiana kuhusu pote hili, pamoja na makosa waliyonayo, hususan, pale mufti aliposema: Pote hili ni ma-Khawaarij, makafiri-wapotofu, Allaah awaangamize waliosalia miongoni mwao katika ulimwengu huu, na kuuvunja msikiti huwo ni wajibu kama ilivyowajibu kuwafukuza kutoka kwenye ardhi za Waislamu."

Nikasema, "bado hatujaafikiana chochote, na wala hatujafika popote katika mdahalo huu… na nitakuonyesha yakwamba ziko fatwa nyingi zinazofanana na hii, tangu hata kabla ya al-Lakhami na baada yake zilizowahi kutokea kutoka kwa Wanavyuoni wa Spain, na Wanavyuoni kutoka Sehemu za Afrika ya kaskazini, na hayo yamekuja kutokana na hukmu ya Mtume wa Allaah (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*) juu ya ma-Khawaarij, wale ambao'Ali ibn Abee Taalib, radhiallaahu 'anhu aliopigana nao huko Nahrawaan.

Na Insha-Allaah katika mdahalo wetu huu, tutawasili kwenye marekebisho ya ufahamu wa kimakosa wa matukio haya ya ki-historia, yanayohusiana na maana ya pote hili, ambalo Wanavyuoni wa ki-Islamu wa Spain na Afrika ya Kaskazini na wenye kufanana nao wametoa fatwa kuwahusu, na kulihusu jina lililoambatanishwa kama kasoro katika kuueleza mfumo wa Da'wah wa marekebisho wa Shaykh Muhammad ibn 'Abdulwahhaab (*Rahimahullaah*). Marekebisho haya hayatoridhisha isipokuwa yaandamane na ushahidi, ambao ni wenye kuwaridhisha nyinyi, kwa sababu ni matumaini yetu sisi sote kuwasili kwenye ukweli wa maudhui haya… na hali njema ya utulivu wa fahamu zetu ndicho kitu kitakacho kutuondolea upofu na kutusaidia katika marekebisho ya kutoeleweka huku."

Akasema, "Sisi sote twataraji kuwasili kunako ukweli…"

Kisha akasema, "na baada ya fatwa hii, tungelipenda nawe utuletee chochote ulichonacho, nasi tutakusikiza, kama watakavyokusikiza ndugu zetu watakaohukumu baina yetu, nao watahukumu yale watakayoletewa mbele yao iwapo ni saheeh au la."

Nikazungumza, "Mutajionea wenyewe, Insha-Allaah lile litakalo ng'arisha njia katika kulifichua jambo hili, kwani yule mwenye kutamani kuwasili katika rai iliyosibu, na kwa hayo: tutaanza na yaliyo mbele yenu kutoka katika juzuu za al-Mi'yaar…

Waweza kutusomea kutoka katika mjalada ili ndugu nao wapate kusikia?

Akasema, "Wamaanisha ile fatwa, yaani niwasomee, au wataka nianze na maelezo yaliyo katika gamba la kitabu??"

Nikasema, "Gamba la nje… au gamba la ndani, vyovyote ni sawa, utakavyo…"

Basi akasoma, "Al-Kitaab al- Ma'rib Fee Fataawaa Ahl al-Maghrib, kilichotungwa na: Ahmad bin Muhammad al-Wanshareesi aliyekufa katika mwaka wa 914H mjini Fez , Morocco .

Nikasema kumwambia Shaykh aliyekuwa na umri mkubwa kutushinda sote pale, nae alikuwa Akiheshimiwa na ni mtu mkarimu, jina lake ni Ahmad, "Ewe Shaykh Ahmad, hebu andika tarehe ya kufa ya muandishi Ahmad al-Wanshareesi…" nae akaandika mwaka ambao ni 914H.

Kisha nikasema, "Twaweza kupata wasifu (Biography) wa al-Lakhami?"

Akasema, "Naam…" kisha akasimama na kutembea kuelekea kwenye rafu (shelf) miongoni mwa ma-rafu ya maktaba na akaleta juzuu moja kutoka katika vitabu vya wasifu, ambayo ndani yake muna wasifu wa: 'Ali bin Muhammad al-Lakhami, ambae ni mufti wa Spain na Afrika ya Kaskazini na wasifu yenyewe ilikuwa ni ndefu, ndani yake muna sifa zake na sifa za daraja yake ya ilimu… Nikasema, "Mwishoni mwa wasifu wake kuna mstari wa mashairi: sasa alikufa lini yeye?"

Aliyekuwa akisoma akasema, "na alikufa katika mwaka wa 478H."

Kwahivyo nikasema kumwambia Shaykh Ahmad, "Hebu andika tarehe ya kufa kwa Shaykh 'Ali al-Lakhami, nae akaandika kama mwaka wa 478H."

Kwahivyo Daktari 'Abdullaah akasema, "kwani wewe una shaka na Wanavyuoni wetu na fatwa zao?"

Nikasema, "Kwani ni kitu gain kilichokutia kwenye shaka hii?... kisha nikawageukia mashekhe… nikasema: "Jamani katika maneno haya kuna mwito wowote kutoka kwangu wa kutia shaka?..."

Basi jawabu likaja, kwa njia ya

(Endelea kwenye Ukurasa wa 3)

NI "UWAHABI" UPI ULIOKUSUDIWA?

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

muafaka, la kukanusha.

Nikasema, "Kwa min-ajil ya kukanusha shaka hii kunihusu mimi, na kutoka kwa Wanavyuoni wa nchini mwangu, kwani sisi twawaheshimu na kuwakirimu, na twazikubali fatwa zao zote kuwa ni za sawa, maadamu zimeandamana na ushahidi kutoka katika kitabu kitukufu na yaliyo saheeh kutoka katika Sunnah za Mtume wa Allaah (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*). Hatahivyo, katika kuwasili kwenye makusudio tuliyoanzia nayo ya mjadala hapo mwanzoni, yamefungamana na mambo aliyoyatumia kama ushahidi wake, na yanahitaji subira na uvumilivu.

Na miongoni mwa mambo yatakayoharakisha jawabu letu ni kwamba: Mimi ningependa kuwauliza kila mmoja wenu suali hili: Jee, yawezekana kwa Wanavyuoni kutoa fatwa kuhusu kanuni za Imani ambazo mtetezi wake, ambae alienasibishwa na kanuni hizo, hata hajaumbwa, au kwamba wahukumu kuhusu pote ambalo hata halijawahi kuwepo??!!"

Wote kwa umoja wao wakasema, "Laa… tena jambo hilo haliwezi kujulikana, isipokuwa yale yaliyokuja kuhusiana nayo kutoka kwa Mtume wa Allaah (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*). Na hayo ni miongoni mwa miujiza ya Utume, ambayo kwa mara nyingi hutajwa kwa njia ya sifa bila ya kutaja jina."

Nikasema, nikiyaelekeza maneno yangu kwa yule niliyekuwa nikizungumza nae, "Kwani wewe huamini, kama wanavyoamini wengine, yakwamba Wahhaabiyyah ilianzishwa na Muhammad bin 'Abdul-Wahhaab huko Najd?"

Akajibu, "Hapana Shaka."

Nikasema, "Kwa hakika, Shaykh Muhammad bin 'Abdul-Wahhaab; wakati al-Lakhami alipotoa fatwa yake, kama jinsi Wanavyuoni wengine wa Spain kutoka katika madh-hab ya Maaliki, na wale wa Afrika ya Kaskazini, palikuwa na zaidi ya vizazi 22 ambavyo hata havijawahi kuumbwa, kwa kudhania yakwamba katika kila karne palikuwa na vizazi vitatu. Kama ilivyo baina ya kifo cha 'Abdul-Wahhaab bin Rustum na kifo cha Shaykh Muhammad bin 'Abdul-Wahhaab palikuwepo na takriban vizazi 31. Na Wanavyuoni wenu, na Wanavyuoni wa Waislamu hawayajui mambo yaliyofichamana (ghayb), na sisi twawajua wao kuwa hawahusiki na mambo ya aina hizo za ramli au uchawi, na kuzungumza mambo wasiyoyajua, kama alivyosema Allaah (*Subhaanahu wata'aalah*): **"Sema: Hakuna aliyoko katika mbingu na ardhi ajuaye Ghayb (yasiyotokea) ila Allaah; nao (hao wanaowaabudu) hawajui ni lini watafufuliwa, (watayajua mengineyo?)."** (An-Naml 27:65)

Akasema: Hebu fafanua zaidi…!!

Nikasema: Kwa hakika Sh. Muhammad bin 'Abdul-Wahhaab alizaliwa katika mwaka wa 1115H, na akafariki katika mwaka wa 1206, na baina yake na Ahmad al-Wanshareesi, aliyeandika kitabu al-Mi'yaar, na yule aliyeinukuu fatwa ya al-Lakhami – kama tulivyowahi kuona, ni miaka 292 kulingana na tarehe walizokufia. Kama ilivyo baina ya Sheikh Muhammad bin 'Abdul-Wahhaab na al-Lakhami, ambae ndiye asili ya fatwa hiyo, kuna miaka 728, kulingana na tarehe za vifo vyao, na kulingana na yale aliyoandika Sheikh Ahmad kuhusu vifo vya kila mmoja wao.

Hapa tunalinganisha; kwa wale wote waliopasisha fatwa hiyo, miongoni mwao wakiwemo wanavyuoni wa Spain na Afrika ya Kaskazini, kuwahusu hawa ma-Wahhaabi…

Akasema: Jee, pana uwezekano wa kuyachambua zaidi makusudiwa yako… na ushahidi wenye kuridhisha?

Nikasema: "Wanavyuoni wa Afrika ya Kaskazini na Spain hawakuhusika katika kutoa fatwa juu ya ma-Wahabi na kuwatahadharisha watu dhidi yao, isipokuwa kwa ajili yakwamba walikuwepo miongoni mwao, kinyume na wao kuwepo katika ardhi nyengine za Waislamu, zenye mapote yaliyotambulika na kubainishwa na ash-Shahrastaani katika kitabu chake kiitwacho al-Milal wan Nihal, kama alivyofanya Ibn Hazm katika kitabu chake al-Fisal Fee al-Milal wal Ahwaa' wan-Nihal.

Amma kuhusu mjadala wetu, unacho kitabu hapo cha al-Firaq al-Islaamiyyah Fee Shimaal Afreeqiyyah, kilichotungwa na Mfaransa: Verdibel, kilichofasiriwa kwa lugha ya kiarabu na 'Abdur-Rahmaan Badawi… nacho ni juzuu moja.

Akasema: "Hiki hapa, ninacho… kisha akasimama na akenda kukichukuwa.

Nikasema, "Tutakisoma karibu na mwisho wake, herufi 'Waaw'"… basi akasoma mojawapo: al-Wahabiyyah au al-Wahhaabiyyah: Khaarijee, pote la 'Ibaadhi lililoanzishwa na 'Abdul-Wahhaab bin 'Abdur-Rahmaan bin Rustum, al-khaariji al-'Ibaadhi, na likaitwa al-Wahhaabiyyah baada ya jina lake. Alizibadilisha Sheriya za Uislamu, na akabatilisha hajj, na kuliwahi kutokea vita mara nyingi baina yake na wapinzani wake…", mpaka akasema: Alikufa katika mwaka wa 197H, katika mji wa Taahirat – katika sehemu za Afrika ya Kaskazini, na akaeleza yakwamba pote hili lilijipatia jina hilo: kwa sababu ya yale waliyozuwa kwenye madh-hab yanayohusiana na 'Aqeedah; na walikuwa wakiwachukia ma-Shi'ah, na kwa chuki za aina kama hiyo waliwachukia Ahl as-Sunnah. Na mtu huyu alisema katika kitabu chake alichokipa sifa kubwa kuhusu mapote ya ki-Islamu ya Afrika ya Kaskazini tangu kushindwa vita kwa Waarabu hadi wakati wa muandishi.

Na kuhusu 'Abdul- Wahhaab bin Rustum kuna ikhtilafu ya maoni, juu ya tarehe ya kufa kwake, kutoka kwa wale walioandika kumuhusu yeye, na az-Zarkili akakisia katika kitabu chake al-A'laam yakwamba alikufa kwenye mwaka wa 190 H.

Kwa hayo, nikasema kumwambia, pamoja na wale waliohudhuria: Huu ndiwo Uwahabi uliougawanya Ummah wa ki-Islamu, na ndiwo ule ambao fatwa hizi, kutoka kwa wanavyuoni na ma-Faqeeh wa Spain na Afrika ya Kaskazini, zilizohusu, kama ambavyo uonavyo katika vitabu vyao vya 'Aqeedah, na wao walikuwa sawa kuhusu waliyo yasema kwenye mas-ala hayo.

Amma kuhusu Da'wah ya Shaykh

NI "UWAHABI" UPI ULIOKUSUDIWA?

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 3)

Muhammad bin 'Abdul- Wahhaab, iliyosaidiwa na Imaam Muhammad bin Sa'ud (*Rahimahullaah*), nayo ni Salafiyyah iliyo saheeh, na tena ni kinyume cha ma-Khawaarij na vitendo vyao, kwa sababu hayo yamethibitishwa katika kitabu cha Allaah, na yaliyosihi kutoka katika Sunnah za Mtume wa Allaah (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*), na inatupilia mbali kila chenye kwenda kinyume na hayo, nayo (Da'wah hiyo) imetokamana na Ahl as-Sunnah wal Jamaa'ah.

Na Shaka zilizopakizwa katika kila pembe ya ardhi za waislamu, zilisambazwa na maadui wa waislamu, wanaotokamana na wakoloni pamoja na wengineo, kwa min-ajil ya kuzua utengamano baina yao, kwani wakoloni walikuwa wametawala sehemu nyingi za ulimwengu wa ki-Islamu katika zama hizo, na huwo ulikwa ndiwo wakati wao wa kujivuna, na waliyajua hayo kutoka kwenye vita vyao vya msalaba yakwamba adui wao wa kwanza katika kuthibitisha nguvu zao, ni Uislamu usiokuwa na doa, kama kielelezo chake katika kufuata mfumo wa Salaf. Kwahivyo wakajionea mtindo fulani wa vazi ambalo litakalo wawezesha kuuvika nalo Da'wah hii ili waweze kuwakimbiza watu, na kuwagawanya waislamu – kwani shabaha yao ilikuwa ni wagawanye ili uwatawale. Na haya ni kwa sababu Salaah ad-Deen al-Ayyoobi (*Rahimahullaah*) hakuwang'oa kutoka katika ardhi za Shaam na hadi sehemu nyengine isipokuwa baada ya kuuangamiza utawala wa Faatimiyyah – Baatini ya 'Ubaydiyyah – walioko Egypt, kisha akawachukuwa wanavyuoni wa Ahl as-Sunnah kutoka ash-Shaam na kuwatawanya katika kila sehemu za Egypt, na matokeo yake Egypt ikabadilishwa kutoka katika Imani ya Baatini ya ki-Shi'ah na kuwa katika njia ya Ahl as-Sunnah, ambayo iliyo wazi katika ushuhuda wake, vitendo vyake na 'Aqee dah.

Kwahivyo wakolono wakahofia kusitokee marudio ya matukio, baada ya kuona yakwambaTaifa la ki-Sunni lililo na msimamo wa Tawheed ; lilo-ongozwa na ma-Imaam wawili: Muhammad bin 'Abdul-Wahhaab, na Muhammad bin Sa'ud, kisha na wale walokuja baada yao – yakwamba ulinganizi wake ukawa unasambaa, na idadi ya wale walioitikia mwito wa Da'wah hiyo ikawa inazidi. Na kama mujuavyo nyote, yakwamba wakoloni hawakuwa na lengo lolote katika kuvamia mji wowote wa ki-Islamu isipokuwa ni kuwatenga Ahl as-Sunnah, na wakajikurubisha na wazushi na wenye kufuata matamaniwa yao, kwa sababu wao ni vyombo vyao vya kuyatekeleza wayapendayo katika nchi za ki-Islamu

FADHLA ZA MWEZI WA MUHARRAM

Amepokea Abu Bakr (رضي الله عنه) kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuwa amesema: "*Hakika zama zinazunguka kama namna yake siku alivyo umba Allaah Mbingu na Ardhi. Mwaka mmoja ni miezi kumi na mbili, katika hiyo kuna miezi minne mitukufu, mitatu ni yenye kufuatana nayo (Dhulqaada, Dhulhijja na Muharram) na Rajab mudhwar ambayo iko baina ya Jumaada na Shaaban.*"

SAUMU YA ASHURA

Hakika usunna wa saumu inakokotezeka katika siku zilizo bora, na siku bora baadhi yake hupatikana kila mwaka. Kama saumu ya siku sita za shawwaal baada ya Ramadhani na kama saumu ya siku ya 'Arafah na siku ya 'Aashurah na siku za Dhul-Hijja na Muharram.

Kupendekezwa katika kufunga mwezi wa Allaah - Muharram.

Imepokewa na Abu Hureira (رضي الله عنه) kuwa amesema, "Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم), *"Saumu bora baada ya Ramadhani ni Mwezi wa Allaah Muharram na swala bora baada ya swala ya Faradhi ni swala ya usiku*".

Imepokewa na Jundub ibn Sufiyyan (رضي الله عنه) kuwa amesema, "Alikuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisema, '*hakika swala bora baada ya swala ya fardhi ni kuswali katikati ya usiku na saumu bora baada ya Ramadhani ni Mwezi wa Allaah ambao wanauita Muharram.*'" Neno la Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Mwezi wa Allaah Muharram"* ameunasibisha kwa Allaah kwa ajili ya kuutukuza pamoja na kuwa miezi yote ni ya Allaah kama alivyosema Allaah (سبحانه وتعالى) "Huyu ni ngamia wa Allaah, (muacheni) na kinywaji chake." Na alikuwa Sufiyan ibn Uyaynah akisema katika neno la Allaah (سبحانه وتعالى): **"Na jueni ya kwamba chochote mnachokiteka(mnacho kipata ngawira) basi sehemu yake ya tano ni kwa ajili ya Allaah."** Amezinasibisha ngawira kwenye nafsi yake kwa sababu ni pato tukufu na hakusema hivyo katika zaka, sadaka hupewa (watu hawa) mafakiri..."

Hakusema zaka ya Allaah ni ya mafakiri kwa sababu zaka ni taka za watu. Na kuitafuta zaka ni makruhu ispokuwa kwa mwenye kuihitaji. Amesema Siddeeq Hassan Khan: "Ama mwezi wa Muharram hapana shaka mwezi huo ni bora ya saumu za sunnah na haizidi katika ubora huo isipokuwa ilivyo sunna katika saumu ya siku ya 'Arafah.

FADHLA ZA SIKU YA 'ASHURAH

Imepokewa na Abu Qatada (رضي الله عنه) kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliulizwa kuhusu saumu ya 'Ashurah akasema, *"hufuta madhambi ya mwaka uliopita."* Na katika mapokezi ya Ibn Majah, Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema, "*Saumu ninataraji kwa Allaah kuwa inafuta madhambi ya mwaka uliopita.*" Amesema Imam Ibn Hubeira katika kitabu chake *Al Ifshwah* Hadithi hii inafahamisha ubora wa mwezi wa Muharram kwa sababu ni mwanzo wa mwaka kwa hiyo aupokee mtu kwa kufanya ibada hutarajiwa kwa hilo ni yenye kufuta madhambi ya mwaka mzima. Na imepokewa kwa Ibn Abbass amesema "Hakuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akikusudia kufunga siku hali ya kutaka fadhla zake ispokuwa saumu ya Ramadhani kutokana na siku hii ya Ashura. Na imeswihi kutokana na Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuwa amesema: "*Saumu ya siku ya 'Arafah hufuta madhambi ya miaka miwili, mwaka uliopita na ujao na Saumu ya siku ya Ashura hufuta madhambi ya mwaka ulipita.*"

[**ENDELEA KATIKA MAKALA YAJAYO**]